

Ghorofa ya Saba, LAPF Pensions Fund Tower; Mkabala na Kijiji cah Makumbusho, Kijitonyama; S.L.P 72175,
DAR ES SALAAM; Simu: +255-22-2923513/8; Nukushi:+255-22-2923519
Barua Pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMILAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA PANGANI ("PAWASA WSSA") KWA MWAKA 2016/17 – 2018/19

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-16-013

Mnamo tarehe 28 Juni 2016 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Pangani (PAWASA WSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2016/17 hadi 2018/19. Hata hivyo, ombi la PAWASA WSSA halikuwa kamili na waliagizwa na EWURA walete viambatisho, taarifa na takwamu muhimu kukamilisha ombi lao. Jedwali namba 1 hadi 6 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei na tozo za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Aina za Wateja	Matumizi	Bei za Sasa	% Ongezeko	Bei Zilizopendekezwa 2016/17 – 2018/19
Majumbani	1 - 5	540	85	1,000
	6 - 10	600	100	1,200
	11 - 30	650	115	1,400
	>30	700	114	1,500
Biashara	1 - 30	740	76	1,300
	>30	790	90	1,500
Taasisi	1 - 30	730	64	1,200
	>30	780	92	1,500
Magati		1200	25	1,500

Jedwali 2: Bei za Sasa na Zilizopendekezwa kwa Wateja wasio na Dira (Shilingi/Mwezi)

Aina za Wateja	Bei za Sasa	% Ongezeko	Bei Zinazopendekezwa 2016/17 – 2018/19
Majumbani	7,400	62	12,000
Taasisi	7,800	67	13,000
Biashara	9,000	56	14,000

Jedwali 3: Ada ya Maunganisho ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi/Maunganisho)

Aina ya Wateja	Ada ya Sasa	% Ongezeko	Ada inayopendekezwa 2016/17 – 2018/19
Majumbani	37,000	8	40,000
Taasisi	37,500	9	41,000
Biashara	38,000	11	42,000

Jedwali 4: Ada ya Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Aina ya Wateja	Ada ya Sasa	% Ongezeko	Ada inayopendekezwa 2016/17 – 2018/19
Wateja Wote	5,500	82	10,000

Jedwali 5: Ada ya Fomu ya Maombi ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi/Fomu)

Aina ya Wateja	Ada ya Sasa	% Ongezeko	Ada inayopendekezwa 2016/17 – 2018/19
Wateja Wote	1,000	200	3,000

Jedwali 6: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi/Mwezi)

Aina ya Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo inayopendekezwa 2016/17 – 2018/19
Wateja Wote	-	500

PAWASA WSSA imeeleza kuwa bei zinazopendekezwa zitaisaidia kumudu gharama za uendeshaji na hivyo kutoa huduma endelevu kwa wateja.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumatano, tarehe 24 Agosti 2016 katika Ukumbi wa Safari Annex kuanzia saa 4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu ndani ya siku 14 baada ya mkutano (**Ifikapo tarehe 7 Agosti 2016**). Maeleo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi ya EWURA, LAPF PENSIONS FUND TOWER; **MKABALA NA KIJIJI CHA MAKUMBUSHO, KIJITONYAMA, DAR ES SALAAM au ofisi za PAWASA WSSA, PANGANI.**

Imetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu
Mamalaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
5 Agosti 2016